## Wizara ya Kazi ya Marekani

## Matokeo ya  Mwaka 2022 kuhusu Aina Mbaya zaidi za Utumikishwaji wa Watoto

# Tanzania

Mnamo mwaka 2022, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanya maendeleo kiasi katika juhudi za kutokomeza aina mbaya zaidi za utumikishwaji wa watoto. Serikali ya Muungano ya Bara ilitoa, kwa mara ya kwanza baada ya miaka kadhaa, habari kamili kuhusu juhudi zake za utekelezaji wa sheria za kazi, ikibainisha matukio 74 ya ukiukwaji wa sheria ya utumikishwaji wa watoto kwa kupitia ziara 4,800 za uchunguzi wa sehemu za kazi. Serikali pia iliunda kikosi kazi kipya cha kuboresha juhudi za kuzuia na kushughulikia jinai za usafirishaji haramu wa binadamu, zikiwemo zile zinazohusisha watoto, na pia ilitenga rasilimali za kifedha ili kusaidia Mkakati wa Kitaifa wa Kutokomeza Utumikishwaji wa Watoto. Hata hivyo, watoto nchini Tanzania hutumikishwa kwa kazi zilizo mbaya zaidi kwa watoto, zikiwemo kutumikishwa katika uchimbaji wa madini, uchimbaji mawe na kazi za majumbaninyumba. Watoto pia hufanya kazi hatari za kilimo. Mapengo mengine yamebaki katika mfumo wa kisheria na utekelezaji wa sheria zinazohusiana na utumikishwaji wa  watoto, ikiwa ni pamoja ukosefu wa adhabu kwa ajili ya utumiaji wa watoto katika shughuli haramu, ukosefu wa kinga ya umri wa chini kwa watoto wanaofanya kazi za nyumba na upungufu wa idadi ya wakaguzi wa kazi ili kufuatilia nguvu kazi ya Tanzania.

**Hatua Zilizopendekezwa za Serikali Kutokomeza Utumikishwaji wa Watoto**

| Eneo | Chombo Husika | Hatua Iliyopendekezwa | Mwaka (Mi) Iliyopendekezwa |
|---|---|---|---|
| Mfumo wa Kisheria | Bara | Panua orodha ya kazi na shughuli hatari zilizopigwa marufuku kwa watoto ili kuhakikisha kwamba orodha hiyo inajumuisha kupalilia na usindikaji kwenye uzalishaji wa tumbaku, karafuu, kahawa, katani, na chai. | 2016 – 2022 |
| | Bara | Haramisha utumiaji wa watoto katika shughuli haramu, hususani katika kuzalisha na kuuza madawa ya kulevya. | 2012 – 2022 |
| | Bara na Zanzibar | Haramisha uandikishaji wa watoto chini ya umri wa miaka 18 unaofanywa na vikundi vyenye silaha visivyo vya serikali. | 2016 – 2022 |
| | Bara na Zanzibar | Hakikisha kwamba kinga za umri wa chini zinawahusu watoto wote, wakiwemo wale ambao wanafanya kazi za nyumba. | 2013 – 2022 |

| Hatua Zilizopendekezwa za Serikali Kutokomeza Utumikishwaji wa Watoto | | | |
|---|---|---|---|
| **Eneo** | **Chombo Husika** | **Hatua Iliyopendekezwa** | **Mwaka (Mi) Iliyopendekezwa** |
| | Bara na Zanzibar | Ongeza umri wa lazima wa elimu kutoka miaka 13 hadi 14 ili ulingane na kiwango cha chini cha umri wa kufanya kazi. | 2017 – 2022 |
| | Bara | Weka kwa mujibu wa sheria, elimu ya bure ya msingi kwa umma na pia ondoa mamlaka ya kisheria ya mamlaka za elimu za ngazi ya chini juu ya kutoza ada za shule kwa hiari yao wenyewe. | 2016 – 2022 |
| Utekelezaji | Bara na Zanzibar | Hakikisha kwamba utaratibu wa malalamiko juu ya kazi kwa watoto una rasilimali za kutosha ili kutekeleza operesheni zao. | 2021 – 2022 |
| | Bara | Ongeza rasilimali za kifedha na idadi ya wakaguzi wa kazi kutoka 87 hadi 643 ili kuhakikisha wanakidhi nguvu kazi ya watu wapatao milioni 25.7 na kuimarisha utambulisho na ufuatiliaji wa vitendo vya ukiukwaji wa sheria za kazi. | 2013 – 2022 |
| | Zanzibar | Ongeza rasilimali muhimu zinazotolewa kwa wakaguzi wa kazi, vikiwemo vifaa vya ofisi, usafirishaji, na mafuta. | 2013 – 2022 |
| | Bara na Zanzibar | Kuza utaratibu wa ukusanyaji na uchapishaji wa pamoja wa data zinazohusiana na aina mbaya zaidi za utumikishwaji wa watoto, ikiwemo idadi ya uchunguzi, na adhabu zilizotolewa kwa ukiukwaji unaohusiana na aina mbaya zaidi za utumikishwaji wa watoto. | 2021 – 2022 |
| Uratibu | Bara na Zanzibar | Hakikisha kwamba Kikosi kazi cha Kitaifa cha Elimu Juu ya Utumikishwaji wa Watoto kinaweza kutekeleza mamlaka yake yaliyokusudiwa. | 2018 – 2022 |
| Sera za Serikali | Bara | Ondoa masharti katika Mtihani wa Kumaliza Masomo ya Shule ya Msingi ambayo ni vizuizi kwa elimu, ikiwa ni pamoja na kuwaruhusu watoto ambao wanafeli mtihani mara ya kwanza kuweza kuufanya tena kwa ajili ya kutiliwa maanani ili kujiunga na shule za sekondari. | 2016 – 2022 |

| Hatua Zilizopendekezwa za Serikali Kutokomeza Utumikishwaji wa Watoto | | | |
|---|---|---|---|
| **Eneo** | **Chombo Husika** | **Hatua Iliyopendekezwa** | **Mwaka (Mi) Iliyopendekezwa** |
| Programu za Kijamii | Bara | Panua taratibu za kurahisisha kujiandikisha tena kwa wasichana ambao wanaacha shule kwa sababu ya kupata mimba. | 2021 – 2022 |
| | Bara na Zanzibar | Imarisha juhudi za kuondoa vizuizi na pia fanya elimu ipatikane kwa watoto wote nchini Tanzania, wakiwemo wale wanaoishi maeneo ya vjijini, kwa kuhakikisha rasilimali za kutosha kwa watoto wenye ulemavu na matatizo ya kujifunza; kuongeza rasilimali kwa walimu, vyumba vya madarasa, madawati, chakula, na vifaa vya usafi wa mazingira; na kuepuka kuzilipisha familia gharama zisizo rasmi, ikiwa ni pamoja na sare za shule, vitabu, na vifaa vingine vya kujifunzia. | 2010 – 2022 |
| | Bara na Zanzibar | Oanisha hatua za kuzuia na kutokomeza utumikishwaji wa watoto na kuziingiza hatua hizo katika Mpango wa Mfuko wa Kijamii wa Uhamishaji wa Fedha Taslimu wenye Masharti ili kuongeza ufanisi wake katika kuzuia na kutokomeza utumikishwaji wa watoto. | 2022 |
| | Bara na Zanzibar | Kuza mipango inayojumuisha kilimo, huduma za nyumba, uvuvi, na sekta zisizo rasmi ili kushughulikia watoto wanaohusishwa katika utumikishwaji wa watoto. | 2017 – 2022 |